MWONGOZO WA KARATASI YA TATU
MTIHANI WA JUNI 2017

SEHEMU A: USHAIRI

1.Maswali

(a) Thibitisha kuwa utungo huu ni shairi (alama 4)
-lina beti nne
-kila ubeti lina mishororo ingawaje idadi inatofautiana katika kila ubeti
-lina mizani katika mishororo

(b) Fafanua toni ya utungo huu (alama 2)
Toni ya kusihi- "nikumbuke mwanangu"
Wosia/nasaha

(c) Huku ukitoa mifano, linganua kati ya mistari toshelezi na mistari mishata (alama 4)
Mistari toshelezi-mstari uliokamilika kimaana ilhali mstari mishata ni mstari usiokamilika kimaana
Mfano wa mstari toshelezi-Nikumbuke mwangu,
Mstari mishata-staftahi ya saa nane alasiri

(d) Eleza maudhui yoyote matatu yanayojitokeza (alama 6)
Umaskini- Mrejelewa na mamake walipitia maisha magumu hapo awali" kumbuka nyakati zile mimi nimamako tulivyojidamka.

Ukengeushi-anafurahia vitu vya kigeni-magari,saa
Ajira-Anarauka asubuhi kwenda kazini
Bidii-Anatia bidii kazini na kuweza kumiliki mali-volvo

(e) Mbinafsi-anajali maslahi yake na kuacha mamake akihangaika
Mwenye bidii-anarauka mapema kwenda kazini
Msomi-aliacha mamake na shughuli na kwendi shuleni.

SEHEMU B: RIWAYA

2.

(a) Msemaji ni Imani
-Msemewa ni Amani
-walikuwa katika kibanda cha Amani
Imani alikuwa akimhadithia Amani sababu ya yeye kusafiri Sokomoko na kutoka nyumbani kwao.

(b) (i) Tashbihi kwa mfano walimpiga kitutu kama nyoka.

(ii) Mbinu rejeshi-Nikumbukapo naona fundo chungu moyoni.

(c) Ukatili/dhuluma

Kuuliwa kwa mamake Imani na kuchomwa kwa nyumba zao

(i) Yusufu anafungwa jela kwa makosa ambayo hakutenda kwa kusingiziwa kifo cha chichiri Hamadi
(ii) Amani anadhulumiwa kwa sababu ya unyonge.Familia yake inanyanganwa shamba
(iii) Amani na Imani kudhulumiwa na askari wa Mtemi Nasaba Bora wakiwa seli
(iv) Mtemi Nasaba Bora kutumia askari kumpiga na kumuua mamake Imani
(v) Amani anaonewa gere na wanafunzi wenzake wanaficha karatasi za uchochezi kwa chumba chake na kugungwa kipindi cha miaka mitatu
(vi) Bob Dj kudhulumiwa na Mtemi Bora kwa kutopelekwahospitali baada ya kung'atwa na mbwa.
(vii) Matuko weye kudhulumiwa na askari wa Mtemi kwa kushikwa kwa nguvu na kupelekwa seli baada ya kusema ukweli kuhusu Nasaba Bora.
(viii) Chwechwe anadhulumiwa na serikali ya Tomoko baada ya kuvunjika fupaja
(ix) Majisifu kumwachia Dora malezi ya watoto wao walemavu

Zozote 12

1x12=12

3.

(i) Barua
-Barua ya majisifu kutoka chuo kikuu cha mkokotoni kumwalika kutoa mhadhara kwa wanafunzi kuhusu kitabu chake cha kidagaa kimemwozea
-Barua ya Ben Bella kwa Mashaka kuvunja uhisiano
-Barua ya madhubuti kwa Mtemi Nasaba Bora kumjulisha kwamba alikamilisha masomo yake na alikuwa tayari kusafiri.Pia alimwambia kwamba asimamishe mipango za kumtafutia kazi.
-Barua ya Lowela kwa Mtemi Nasaba Bora akimtishia kutoboa siri asipowaachilia Amani na Imani
4x1=4
(ii) Kinaya

_ Ni kinaya kwamba uso wa Imani unaonyesha tabasamu ilhali moyoni ana huzuni

-Ni kinaya kwamba Mitchelle anamwagiza Majununi kujenga jumba kubwa baadaye anaikataa

-Kinaya kwamba zahanati ya Nasaba Bora inajulikana kama mahali watu wameenda kufia badala ya kupata nafuu..kwa mfano kitoto uhuru

-Nasaba Bora anamwamba Amani kuwa ni mwizi ilhali yeye ndiye

4x1=4

(iii) Sadfa

-Imani na Amani wanakutana kisadfa ziwa Mawewa wote wakiwa safarini kuelekea sokomoko kusaka ajira.

-Imani na Amani wanakutana na Bob Dj pale mto kiberenge na anawapeleka kwa ndugu wawili Nasaba Bora na majisifu

-Amani na Imani wanafika sokomoko kwa Nasaba Bora anapohitaji mchungaji na majisifu kijakazi

_Amani kupatikana na Nasaba Bora chumbani wakiwa na mkewe Bi.Zuhura.

4x1=4

Mbinu rejeshi

(a) Kisa cha Mitchelle na Majununi tunaona usaliti wa Mitchelle
(b) Kisa cha Imani kusimulia Amani kifo cha mamake na kuchomwa kwa nyumba yao
(c) Kisa cha mtemi kununua gari jipya na kumuua paka aliyekula nyama
(d) Tunarudishwa nyuma kurejelea mwiko wa kunywa maji yam to Kiberenge.
(e) Mtemi Nasaba Bora anakumbuka maisha yao wakiwa wadogo babake akiwa kasisi

Majazi

Madhubuti- maana kitu chenye Imara.Anakataa kutafutiwa kazi kwa njia ya hongo.

Majisifu-Ni majigambo.Anajiona kuwa mwandishi maruufu na bora kisarufi

Mashaka-Taabu.Anaachwa na Ben Bella na hata kuwa wazimu

Amani-Mtulivu.anamsamehe Mtemi Bora baada ya kujua ukweli na kutolipiza kisasi.

4x1=4

SEHEMU C: TAMTHILIA

<u>Tamthilia ya Mstahiki Meya</u>

4. (a)

- Msemaji ni Diwani III/Bw. Kheri/Bw. Uchumi
- Anamwambia Meya Sosi
- Walikuwa ofisini kwa Meya
- Meya alikuwa amemwita kutaka atekeleze nyongeza ya mishahara ya wafanyakazi
- Meya anadai kuwa uwakilishi/udiwani ulikuwa kazi

(b) Wahusika hawa ni Meya na Diwani III

- Meya ni katili-anatumia askari kuwapiga na kuwatawanya wafanyakazi wanaodai haki. Diwani III ni mwenye utu- anajali maslahi ya wafanyakazi na kutaka wasikilizwe
- Meya ni mbaguzi/mwenye mapendeleo- anawaongeza madiwani mshahara na kuwapuuza wafanyikazi. Diwani III ni mpenda usawa- anapendekeza madiwani na wafanyakazi wapate nyongeza wote.
- Meya ni mwongo/mdanganyifu- anadai dawa zimeagizwa na zi njiani zaja. Diwani III ni mkweli. Anaeleza wazi kuwa ahadi za Meya za kuagiza dawa zilikuwa ni uongo.
- Meya ni mwoga. Anaogopa kutiwa kizuizini. Anaposhikwa na askari anazimia. Diwani III ni jasiri/mkakamavu- anapinga waiwazi maamuzi ya kueneza propaganda kuwa Baraza la Cheneo limejitolea kuwaletea demokrasia
- Meya ni mwenye kiburi/majivuno- anadai kuwa wanacheneo wanaridhika naye na wangeendelea kumchagua. Diwani III ni mwenye heshima/mnyenyekevu- kila anapokutana na Meya, anamwita MstahikiMeya. Anapopinga hoja anafanya hivyo kwa heshima na kutoa sababu za kuridhisha.
- Meya ni msaliti- anawasaliti wanacheneo kwa kutowapatia mahitaji yao ya kimsingi kama vile chakula, elimu bora, matibabu na kazi. Diwanii III ni mzalendo- anapinga maamuzi yanayochangia kufilisi hazinz ya baraza/ufujaji wa mali ya umma.
- Meye ni mjinga- hatambui unafiki wa Bili na Diwani I na II. Hawa wanamdanganya ili wafaidi. Diwani III ni mwerevu- anatambua kuwa watu wameerevuka na lazima uongozi uweze kutahadhari. Anatambua Meya anapofushwa na viongozi wanafiki.
- Meya ni fisadi- anatumia cheo chake ili kunyakua viwanja vinane na kumgawia rafikiye Bili vinne. Diwani III ni mwadilifu- anakataa kushiriki njama za Meya na madiwani wenzake kufilisi Baraza.
- Meya ni mbadhirifu- anatumia fedha za umma ovyo. Anashiriki starehe katika hoteli, kuidhinisha malipo haramu na kuandaa sherehe ghali. Diwani III ni mwangalifu/mwekevu- anapinga matumizi mabaya ya pesa za umma kwa mfano nyongeza ya mishahara kwa madiwani na kutotozwa kodi kwao
  (Hoja zozote 8x2= 16)

5.

(i) Alidanganyika kuwa,vikosi vya usalama vingeweza kukabiliana na alivyodahi Diwani 1.Matokeo ni maji kuzidi unga na hali ikawa haidhibitiki tena.
(ii) Meya alidanganyika kuwa,kwa kuazisha tamasha za kushindania zawadi,hili lingeamsha uzalendo wao.Jambo hili halikuweza kuamsha uzalendo kwani wananchi walikuwa na matatizo ambayo hayakusuluhisha.
(iii) Meya alidanganyika kuwa,kuwateua asilimia sabini ya madiwani kungeleta ugwaji mkono.
(iv) Meyaalidanganyika kuwa kuwaongezea mishahara walinda usalama kungefanya wawe na moyo wa kutenda kazi na kuwa wazalendo
(v) Meya alidanganyiko kuwa aliungwa mkono na wengi
(vi) Meya alidanganyika kuwa baraza lake ndilo lenye udhabiti mkubwa
(vii) Meya alidanganyika kuwa,kwa kuanzisha tamasha za vijana kushindania zawadi ili kuonyesha uzalendo.Jambo hili halikuhimarisha uzalendo
(viii) Meya alidanganyika kuwa,cheneo kuna amani na utulivu ulioletwa watu wenyewe kutopenda matata.Ukweli ni kwamba amani ilikosekana cheneo na mji ukawa haukaliki kwa fujo na mapambano ya waandamanaji na polisi
(ix) Meya alidanganyika kuwa,kutishia kuwafuta wafanyakazi waliogoma kungewafanya kohofia kupoteza kazi na hivyo waache kugoma.
(x) Meya alijiambia kuwa wanafuata malengo ya millennia.Haya ni malengo ambayo hayakuifaidi.

Zozote kumi

10x2=20

SEHEMU D:HADITHI FUPI

6.

(a) Msemaji –msimulizi
Anawarejelea akina mama wa Kitantele ambao wanapomwona msemaji.Ameandamana na babu yake ambaye ni mweusi. Wanamshuku kuwa amemwiba mtoto wa Kitantele,kwa hivyo wanaanza kujadiliana.Mahali ni katika mtaa wa kochokocho.

(b) Babu wa msemaji alipigwa
Msemaji alibebwa hobelahobela hadi kwa kibanda kimoja
Babu wa msemaji kule nje alipigwa kitutu akauawa na mwili wake kuteketezwa

Ubaguzi

Kuna ubaguzi katika ndoa.Ndoa kati ya watantele na watu makabila mengine zilikuwa ni nadra sana nchini.Kwa hivyo,ndoa kati ya Mama wa msemaji na babake ilipigwa kutoka pande zote mbili.

Utabaka
Kuna tabaka la maskini na matajiri-maskini wanaishi katika mitaa ya mandongoporomoka ilhali matajiri waliishi katika mitaa bora.
Maskini wanaishi katika vyumba duni kama vile msemaji alimotupwa na katika mazingira machafu.
-Kuna tofauti kati ya mjini na kijijini.Mijini kuna huduma bora za afya ikilinganishwa na vijijini.

7. (a) Ufaafa wa anwani **Shaka ya Mambo**

Shaka ni hali ya kutokuwa na hakika ya jambo.Pia huitwa wasiwasi

(i) Esther ana shaka kwani hajabadilisha zamu tangu aambiwe na Grace kuwa atakuwa akibadilisha kila mwezi.
(ii) Esther hana kazi maalum ya kudumu na ana shaka ya vile ataweza kuyakabili maisha
(iii) Esther ana shaka kwani hajui kama uhusiano wake na Kamata wa kutoka zamani.
(iv) Esther ana shaka ya kukatiwa simu na Kamata kila anapompigia simu.anashindwa ni kwa nini Kamata anamkatia simu.
(v) Mteja mzungu ana shaka ya kuachwa na ndege kwani safari yake ilikuwa imeahirishwa mara mbili.
(vi) Esther ana shaka kwani Grace ana miadi muhimu ya nani jioni hii ya saa kumi na moja.Anaambiwa ashike zamu ya mchana na kuwa atalipwa

Zozote tano

5x2=10

(b) Jazanda katika hadithi ya kikaza
Kikaza ni kipande cha chuma cha kuunganisha vipande vya mbao au chuma.Neno hili limetumika kijazanda.Jazanda ni matumizi ya lugha fiche kuwasilisha ujumbe.

(i) Baadhi ya mawingu huwa na maji mabaya.Hii inamaanisha baadhi ya vitedo vya viongozi huwa havina faida kwa umma.

(ii) Si kila panapo mawingu meusi mvua hunyesha.Hurejelea viongozi ambao mara nyingi huonyesha umma eti wako tayari kuleta maendeleo,lakini umma huja kutamauka kwa sababu ya uzembe wao.

(iii) Jazanda ya kikaza pia hurejelea makubaliano au maafikiano (katiba) yanayobainisha na kudhibiti nguvu za watawala.

(iv) Hadithi za kobe kuanzia manyoya na safari kwenda mbinguni,inaashiria viongozi wabinafsi na walaghai.wao hupandishwa madaraka na umma,wao huanza kujifaidi wao wenyewe na kwasahau raia.

(v) Kikaza pia hurejelea wadhifa muhimu katika jamii kama vile uongozi.

(vi) Kikaza pia hurejelea jambo ambalo huleta ushirikiano na utangamano katika jamii

Zozote tano

5x2=10

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8.Linganua fasihi simulizi na fasihi andishi (alama 5)

- Zote mbili zina tanzu mbili kuu ambazo ni fani na maudhui
- Zote huwa na dhima sawa kwa mfano kuelimisha jamii
- Zpote huburudisha
- Zote huwa na fanani na hadhira
- Huzaliwa, hukua na hata kufa kutegemea mabadiliko ya wakati.
- Zote zinaweza kukashifiwa na wasanii mbalimbali ikiwa hawajaridhishwa na mbinu za lugha zilizotumika.
  (5x1=5)

1. Taja asili ya lakabu (alama 5)
   - Tabia za mtu/mhusika
   - Sifa za kimaumbile
   - Matendo ya mhusika
   - Nasaba atokayo mtu
   - Tabaka la mtu
   - Jinsi mtu anavyotamka maneno
     (5x1=5)

2. Onyesha sifa tano za maghani. (alama 5)
    - Huwa na sifa za kishairi (mapigo ya kimuziki, maneno teule na yenye muwala)
    - Hutolewa namtu mmoja au kundila watu
    - Hutungwa kwa ufundi mkubwa
    - Baadhi hutunwa papo hapo na kutolewa mbele ya hadhira
    - Husimulia matukio kwa kirefu
      (5x1=5)
3. Huenda mtafiti akapatwa na changamoto nyanjani. Fafanua.(alama 5)
    - Gharama ya utafiti - Huenda akakosa pesa za kusafiria au hata kununulia vifaa.
    - Kutokana na mtazamo hasi wa jamii, huenda wakakosa kujaza hojaji
    - Huenda akashukiwa kuwa mpelelezi na wakakataa kutoa habari
    - Mtafiti huenda akatatizika iwapo wahojiwa watadai kulipwa
    - Mtafiti huenda akajipata katika vizingiti vya kidini na hivyo akakosa kupata taarifa.
    - Vifaa vya kazi huenda vikapotea au hata kuharibika
    - Uchache wa wataalamu wa kazi za fasihi simulizi na hivyo mtafitikukosa taarifa muhimu
    - Ukosefu wa wakati wa kutosha kuwahoji watu wengi
    - Ukosefu wa usalama

Tatizo la uchukuzi na mawasiliano